JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OR – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI

MKUU WA SHULE: +255786036520/+255620616680
MAKAMU: +255 785672399+255655672399

MHASIBU: +255716570609/+255752787083

Barua pepe : ikwiririss2020@gmail.com

S. L . P 75

IKWIRIRI

TANZANIA

KUMB.NA. ED/ISS/VOL.II/ADV 03

MZAZI WA ……..

S. L. P ……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha TANO 2022/2023 katika shule ya Sekondari Ikwiriri katika Tahasusi ya HKL/HGK…… Tunampongeza kwa mafanikio hayo. Shule itafunguliwa tarehe ……na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe…… Shule ya Sekondari Ikwiriri ipo katika Mkoa wa Pwani umbali wa kilomita 160, Kutoka Dar-es-Salaam. Kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara) washuke Ikwiriri stendi uliza ikwiriri sekondari na utaletwa hadi shuleni. Kwa wanafunzi wanaotoka mikoa mingine wafike MBAGALA rangi3 bus terminal – DSM, ndipo watapata magari ya moja kwa moja kuelekea Ikwiriri, na washuke kituo kinachojulikana ikwiriri stendi(terminal). Uliza Ikwiriri sekondari utaletwa hadi shuleni kwa usafiri wa bodaboda. Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo

A. Maelezo Maalumu Ya Kujiunga Na Shule
B. Ada na michango mbalimbali ya shule.
C. Sheria,Kanuni na taratibu za shule
D. Fomu ya ya Afya (Mwanafunzi apimwe na ijazwe na Daktari aliyemhudumia)
E. Ahadi/Kiapo cha mwanafunzi.
F. Vitabu

Ni matumaini yetu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote Mzazi/Mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.Kama kuna changamoto au maswali yeyote unaweza kupiga namba simu kwa namba zilizoainishwa hapo juu.

Tunakukaribisha sana

…….

NURU .S. MNIKU

MKUU WA SHULE

A: MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE

1 SARE ZA SHULE ZINAZOPATIKANA SHULENI

NB: *Uje na pesa taslimu (Cash) utalipia shuleni na usilipie benki*

a. Sketi rangi ya orange 2 @ Tsh 25000/=
b. Sketi moja ya kijani kwa ajili ya kushindia (shamba dress) Tsh 25000/=
c. T-shirt moja yenye nembo ya shule Tsh 15000/=
d. Nembo(logo) ya shule @ Tsh 3000/= kwa ajili ya kuweka kwenye mashati/nusu kanzu za shule
e. Jezi za michezo (T-shirt na bukta) rangi ya bluu zenye nembo ya shule zote kwa Tsh 10000/=

II UTAKAZONUNUA NYUMBANI:

a. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe na visigino virefu (Jozi 2)

b. shati nyeupe mbili mikono mirefu /nusu kanzu mbili na hijabu yake kwa wanaotaka

c. Soksi jozi 2 au zaidi nyeupe.

d. Viatu vya michezo na kushindia (raba rangi yeyote)

e. Kandambili kwa ajili ya kuogea tu.

f. mtandio/juba rangi nyeupe au pinki kwa ajili ya kushindia kwa wanaovaa hijabu

g. Sweta moja la Bluu

h. Kila mwanafunzi lazima aje na Tracksuti ya blue ambayo ataivaa siku za mwisho wa wiki.

i. sketi nyeusi 1 yenye mshono wa V mbele iwe na urefu wa kuvuka magoti(utavaa wakati unapokuja kuripoti shuleni

NB: *mwanafunzi atapokelewa endapo atavaa uniform (sare) za shule wakati wa kuripoti,mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa shuleni*

2. MAHITAJI YA BWENI

i. Godoro la nchi 2.5 Kwa 6

ii. Shuka rangi ya sky blue Jozi mbili

iii. Mto na foronya 2 za sky blue

iv. Taulo

V. Nguo za ndani/chupi Zaidi ya 12

vi. Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko lita 10

vii. Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili (tranker)

viii. Vyombo vya chakula, Sahani, Bakuli,Kikombe, Kijiko, Chupa ya chai anaweza kuja na ''HOT POT'' 1 ndogo kwa ajili ya dharura za kiafya. Visiwe vya plastiki

ix .Chandarua futi 3x6. Ya pembe nne.

x. Vifaa tiba kwa ajili ya kujikinga na kujilinda na magonjwa kulingana na jinsia yake na hali yake kama

vile Barakoa za kutosha rangi ya orange

3. MAHITAJI YA TAALUMA/DARASANI

a) Rimu 3 kwa mwaka A4

b) Result slip ya kidato cha nne, Cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving Certificate). Halisi na nakala

c) Cheti cha kuzaliwa halisi na Nakala

d) Madaftari 08 (Counter Book) ,Kalamu/Penseli za kutosha

f) Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma Geography.

g) Faili 2 kwa ajili ya kuhifazia mitihani na kumbukumbu zingine ''Folder file''

h) Graph pad moja kwa wanafunzi wanaosoma Geography

MAHITAJI MENGINE

a. Kwanja na fagio laini (softbloom)
b. Fagio la chelewa(kufagilia nje)

B: ADA NA MICHANGO MBALIMBALI:

JEDWALI LA AINISHO LA ADA NA MICHANGO KWA KIDATO CHA TANO

SN	MICHANGO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA
1	ADA	35,000/=	35,000/=	70,000/=
2	KITAMBULISHO	6,000/=	-	6,000/=
3	BIMA YA AFYA	5,000/=	-	5,000/=
4	HUDUMA YA KWANZA	5,000/=	-	5,000/=
5	TAALUMA	20,000/=	-	5,000/=
6	TAHADHARI	5,000/=	-	5,000/=
7	UKARABATI WA SAMANI	15,000/=	-	15,000/=
8	WAPISHI , WALINZI NA VIBARUA	30,000/=	-	30,000/=
9	NEMBO YA SHULE	2000/=	-	2000/=
10	MITIHANI YA MOCK KIDATO CHA TANO	20,000/=	-	20,000/=
JUMLA NDOGO KWA MUHULA WA 1		**143,000/=**		
JUMLA KUU ADA NA MICHANGO INAYOLIPWA BENKI				**178,000/=**

NB: Kwa muhula wa kwanza malipo ya benki yalipwe kwenye akaunti namba ifuatayo

Tsh 143,000/= kwa muhula wa kwanza au Tsh 178,000/= kwa mwaka ILIPWE KWENYE AKAUNTI NAMBA **21301100032 NMB** JINA LA AKAUNTI IKWIRIRI SEKONDARI SCHOOL REC EX

Utapata huduma katika tawi lolote la Benki ya NMB Tanzania.Kuwa makini katika kuweka fedha katika akaunti za shule,fedha ya Ada na michango mengine Tsh 143,000/= iwekwe kwenye akaunti ya benki uliyopewa Hatutahusika na uzembe wowote wa kuchanganya malipo katika akaunti ya shule.Jina la mwekaji liwe la mwanafunzi na si mzazi/mlezi.Mwanafunzi aje na PAY INSLIP ya benki wakati wa kuripoti shuleni.Mwanafunzi aliyekamilisha malipo ya Ada na Michango ndiye atakaepokelewa shuleni na kupewa kadi maalumu ya utambulisho hapa shuleni.

C: SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA kwa ujumla Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri Kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi
   (a) Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya.
   (b) Kufuga kucha na nywele
   (d) Kunyoa kipara
   (e) Kumpiga mwenzake/kupigana
   (f) Kutukana
   (g) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   (h) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, Kwa kuwa Shule hii ni ya Serikali.
   (i) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
   (j) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule
   (k) Kuvaa sketi chini ya kiuno
   (l) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model
4. Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu Kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk
7. Mwanafunzi LAZIMA awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo Mwanafunzi:
   A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba, Mikutano ya darasa na Maabara za shule.
   D.kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya Alasiri (9;30-11:30) NA usiku kuanzia saa

2;00-5;00 .Siku ya Jumamosi maandalio ya masomo yataanza saa 4 asubuhi hadi saa 7 mchana

8. Ni LAZIMA mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na KITAMBULISHO kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:-

9. Jumapili ya Mwisho wa mwezi ni siku ya wanafunzi kwenda kupata mahitaji yake muhimu kuanzia 6 mchana hadi saa 8 Mchana.Zingatia muda na haupaswi kwenda sehemu nyingine yeyote bila Ruhusa.

10. Ni LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, anaapaswa kuwa na kibali (Pass) cha maandishi.(Kilichotolewa na Mkuu wa shule au Mwalimu wa Zamu)

11`. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia electrical heater au jiko la aina yoyote

12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhutasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.

13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi Kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.

14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule ya sekondari ikwiriri muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati au T shirt yake. Mavazi ya nyumbani Hayaruhusiwi kabisa.

15. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama laini, Charger earphone, Ipadi nk.

16. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

17. MAENEO YASIYORUHUSIWA: Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu

- Ofisi za shule
- Chumba cha wafanyakazi
- Maabara
- Jikoni
- Nyumba za wafanyakazi
- Nyumba za ibada
- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe
- Majumba ya kufikia wageni

18.BWENINI

- Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi wa kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake
- Mwanafunzi lazima awepo bwenini kwenye ukaguzi kila siku ya jumamosi asubuhi.
- Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote bwenini wakati wote.
- Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali aliyokabidhiwa bwenini
- Ni marufuku kupeleka viti ,meza na chakula Bwenini.

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI AU KUSIMAMISHWA SHULE:

1. Wizi

2. Uasherati, ushoga na ulawiti.

3. Ulevi wa aina yoyote.

4. Utumiaji wa madawa ya kulevya km vile uvutaji wa Bangi,Cocaine ,Mirungi,Kubeli nk.

5. Uvutaji wa sigara au Bangi

6. Makosa ya jinai

7. Kuoa au kuolewa

8. Kuharibu Kwa makusudi Mali ya umma.

9. Kupigana au kumpiga mwingine.

10. Kudharau Bendera ya Taifa

11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule

12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma Kwa namna yoyote

13. Kutoa lugha ya matusi

14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla

15. Kutohudhuria vipindi

16. Ubakaji.

17. Kuwa na simu ya mkononi.

MAMBO MENGINE YA MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- Medical examination formu ambayo itajazwa na mganga wa Hospitali ya Serikali mara tu atakapowasili shuleni na kuikabidhi.
- Fomu ya Melezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai
- Fomu ya mzazi kukiri kukubalina na sheria ,kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OR – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI

MKUU WA SHULE: +255786036520/+255620616680 .

MAKAMU: +255 785672399/+255655672399

MHASIBU: +255716570609/+255752787083

Barua pepe : ikwiririss2020@gmail.com

S. L . P 75

IKWIRIRI

TANZANIA

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi…….adm.Na……

Kidato ……mchepuo…….mwaka……

Tarehe ya kuzaliwa……

Kabila la mwanafunzi…… Uraia wa mwanafunzi……

Tarehe ya kujiunga na shule ya sekondari ya Ikwiriri……. Shule aliyotoka ya sekondari……

Masomo utakayokuja kusoma…… Kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu……

Je unarudia kidato?…… kwa nini?.....

Dini ya mwanafunzi……Dhehebu……

Anwani ya kudumu ya mwanafunzi S.L. P……..
Wilaya……. Mkoa…….
Tarafa……Kata……..
Kijiji……Namba ya nyumba…… Simu ya nyumbani…… Simu ya ofisini……

BABA

Jina la Baba…… Je,yu hai ?……..

Kabila la baba……Anwani yake ya sasa……
Kazi yake…… Mwajiri wake……

Dini ya baba ……..dhehebu……

Je,baba na mama wanaishi pamoja?..... 21. Simu ya baba……..Ya kazini……

MAMA

Jina la mama…….

Je,yu hai?..... 24. Kabila la mama……

Mwajiri wake ……..

Anwani yake ya sasa……

Dini ya mama……Dhehebu……

Kazi yake ……mwajili wake……

Simu ya nyumbani……Ya ofisini…….

MLEZI

Jina la mlezi……

Kabila la mlezi…….

Uhusiano na mwanafunzi ukoje?..... Anwani ya sasa……

Kazi yake…… Mwajiri wake……
Dini ya mlezi……Dhehebu……

Simu ya nyumbani……..Ya kazini……

NDUGU WENGINE

SN	JINA	ANWANI	SIMU	UHUSIANO

PICHA ZA NDUGU WENGINE

HABARI NYINGINEZO KAMA ZIPO

……
……

Sahihi ya mwanafunzi……. **Tarehe……**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART 'A'

FROM……

TO THE MEDICAL OFFICER …… …….. …… ……..

Mr./Miss……(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl student ineligible for studies.

I (a) Eyesight (e) Venereal Diseases (b) Hearing (f) Leprosy (c) Speech (g) Epilepsy (d) Limbs

II Neuroses

III Other serious diseases

Date…… Signature……

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight…… (e) Venereal Diseases……

(b) Hearing……. (f) Leprosy……..

(c) Speech ……. (d) Limbs……

II Neuroses…….... III Other serious diseases……

Date……Signature…….... Station……..

Designation……

E. AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi …… Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI KIDATO CHA TANO Mchepuo wa …….. mwaka 2022 ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya Bweni Ikwiriri.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma Kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo changuliwa kusoma
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu. …… (Jina la mzazi) Kwa ajili ya hatua zaidi. Saini ya mwanafunzi …… Tarehe ……

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi …… ninakubali mtoto wangu …… Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari ikwiriri mwaka 2022. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa. Anuani yangu ya kudumu ni …… Simu …….. Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/Mlezi ……Tarehe ……..

''TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

F.VITABU

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na baadhi ya vitabu kutokana na masomo (Mchepuo) anayokuja kusoma hapa shuleni.Mwanafunzi atakaguliwa vitabu hivi mara tu atakapofika shuleni

1. GENERAL STUDIES
   Kila mwanafunzi lazima aje na kitabu cha somo la General studies kati ya General studies for A' LEVEL Written By Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratus
2. GEOGRAPHY
   Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Geography anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya
   - Physical Geography by Monk House
   - Practical Geography for Africa By John Richard
   - Fundamental Geography By Josephat

3. HISTORY
   Kila mwanafunzi anayekuja kusoma somo la History anatakiwa kuja na vitabu japo viwili kati ya
   - Essential in Advanced level History paper 1 By Saleh Yassin
   - Advanced Level history Paper 1 By Zisti Kamili
   - The Evolving World By Denis Ngalula
   - Advanced level History Paper Two By Pascrates Fidelis Rutta

4. ENGLISH LANGUAGE
   Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kuja kusoma somo English Language anatakiwa kuja na vitabu viwili kati ya
   - Advanced English Oxford Dictionary 7th Edition (Lazima aje nayo)
   - Introduction to literature by Chace .W.M & Collier
   - Essential English language two second edition by Filbert Kabila & JULIUS Mombeki
   - English language One Form five & six By Kadeghe M

NB; *mwanafunzi anatakiwa pia kuja na angalau vitabu viwili vya PLAY,vitabu na vitabu Viwili vya*

NOVELS

NOVELS

- Divine Providence (severin N.Ndunguru)
- Encounters from Africa (Macmilan Education Limited)
- His excellency the Head of state (Danny Safo)
- The beautiful ones are not yet born (Ayi kwei Arman)
- A man of the people (Chinua Achebe)

PLAY

- Betrayal in the city (Francis Imbugha)
- I will marry when Iwant (Ngugi wa Thiongo)
- The bride (Austin Bukenya)
- An enemy of the people (Henrick Ibsen)
- Black Mamba (John Luganda)

12. KISWAHILI

Kila mwanafunzi aliyepangwa kuja kusoma somo la Kiswahili anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Kiswahili kidato cha 5 na 6 kiswahili 1 Lugha na Sarufi (taasisi ya elimu tanzania) 2019
- Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 (Kilangi Enock LUCAS)
- Tafsiri na Ukalimani (Mwansoko)
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI) Lazima aje nayo Vile vile mwanafunzi anayesoma Kiswahili anapaswa kuja na vitabu vya RIWAYA viwili,MASHAIRI viwili na TAMTHLIYA viwili (**Chagua hapo chini kwenye orodha)**

USHAIRI

- Kimbunga (Haji Gora)
- Mapenzi Bora (Shabani Robert)
- Chungu Tamu (Theobald A Mvungi)
- Fungate ya Uhuru (Mohamedi S Khatibu)

RIWAYA

- Usiku utakapokwisha (Mbunda Msokile)
- Kufikirika (Shabani Robert)
- Mfadhiri (Hussein Tuwa)
- Vuta N Kuvute (Shafi Adam Shafi)

TAMTHILIYA

- Kwenye ukingo wa Thim (Ebrahim Hussein)
- Morani (Emmanuel Mbogo)
- Nguzo Mama (Penina Mhando)
- Kivuli kinaishi (Said Mohamed)